



Dhikiri bora ni: Laa ilaaha Illa Ilaah: Na dua bora ni: Al-hamdulillah

Imepokelewa Kutoka kwa Jabiri -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake amesema:
Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake- akisema:
"Dhikiri bora ni: Laa ilaaha Illa Ilaah: Na dua bora ni: Al-hamdulillah".

[Ni nzuri]

Anatueleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa dhikiri bora ni: "Laa ilaaha illa Ilaah" Na maana yake, hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, nakuwa dua bora ni "Al-hamdulillaah"; Nayo inamaanisha kukiri kuwa mneemeshaji ni Mwenyezi Mungu -Aliyetakasika na kutukuka-, mwenye kustahiki sifa nzuri zilizokamilika.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3567>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

